



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS



TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA

Unapojuibu tafadhali taja:

Kumb:HWR/K.2/15/146

04/08/2023

Mkurugenzi Mtendaji (W)

Halmashauri ya Wilaya

S.L.P 51

Ruangwa

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Kwa mujibu wa kibali cha Ajira Mbadala chenye kumb.Na FA.170/375/01"A"/125 cha tarehe 28 Juni, 2023 kutoka kwa katibu Mkuu (UTUMISHI) Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa anawatangazia nafasi za kazi Watanzania wenyewe sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi Mtendaji kijiji daraja la III

❖ MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III-(NAFASI 3)

A. Sifa:

Mwomboji awe amefaulu kidato cha nne (IV) au Sita (VI) aliyefaulu mafunzo ya Astashahada/Cheti" NTA Level 5" katika moja ya fani zifuatazo:-

Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya jamii kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

B. KAZI NA MAJUKUMU YA AFISA MTENDAJI WA KIJIJI III

- 1) Kukusanya mapato ya Halmashauri ya Wilaya
- 2) Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya kijiji
- 3) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa rai na mali zao, kuwa mlinzi wa amani, Msimamizi wa Utawala bora katika kijiji.
- 4) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji
- 5) katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji
- 6) kutafsiri na kusimamia sera,sheria na taratibu
- 7) kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- 8) kiongozi wa wakuu wa vitengo vyta kitaaluma katika ngazi ya kijiji
- 9) kusimamia kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nvaraka za Serikai ya kilili

- 10) Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika kijiji
- 11) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata
- 12) Kutekeleza shughuli nyingine atakazopangiwa na Mwajiri

D. NGAZI YA MSHAHARA

Cheo cha Mtendaji wa Kijiji daraja la III kina ngazi ya Mshahara TGS B

E. MASHARTI YA JUMLA

- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono na kutumwa kwenye anuani iliyotajwa hapo chini.
- Mwombaji aambatanishe nakala za vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa, maeleo binafsi (CV) na nyaraka zote muhimu pamoja na picha mbili (2) (Passport size) zilizopigwa hivi karibuni.
- Testimonials "provisional results" "statement results" hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (**FORM FOUR AND FORM SIX RESULTS SLEEPS HAVITAKUBALIWA**)
- Nafasi ya kazi iliyooombwa iandikwe juu ya bahasha, kutozingatia hii kutasababisha maombi ya kazi kuwa batili
- Kwa wale watakaopita kwenye mchujo wa awali (short listened candidates). Ndio watakaoitwa kwenye usaili (interview) na kufika na vyeti halisi pamoja na kitambulisho(NIDA/Mpigakura/leseni ya udereva/Kitambulisho cha kusafiria).
- Barua zote za maombi ziandikwe na kutumwa kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA,
S.L.P 51,
RUANGWA**

NB; Uwasilishaji wa barua za maombi kwa mkono katika ofisi za Halmashauri ya Wilaya hazitapokelewa.

Mwisho wa kutuma na kupokea maombi ni tarehe 14th Agosti, 2023 saa 9:30 Alasiri.



Ernest G. Haule

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W).
RUANGWA